

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA WAZIRI MKUU  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE  
YA SEKONDARI TANDAHIMBA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI



Namba za Simu.....

Mkuu wa Shule 0785 270 772

Makamu Mkuu wa Shule 0686 163 188

Shule ya Sekondari Tandahimba

S.L.P 74,

Tarehe.....

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi .....

S.L.P .....

Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA  
SEKONDARI TANDAHIMBA HALMASHAURI YA TANDAHIMBA MKOA  
MTWARA MWAKA.....

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka..... na atasoma tahasusi ya .....

Shule ya Sekondari Tandahimba ipo umbali wa Kilometa 03 Magharibi mwa Mji wa Tandahimba Usafiri unapatikana katika kituo cha mabasi. Nauli ni Shilingi 2,000/- kwa pikipiki na Shilingi 3,000/- kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ..... hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ..... Mwisho wa kuripoti ni tarehe .....

2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-
  - 2.1 Sare za Shule

- i. Sare ya shule hii ni shati nyeupe mikono mirefu na suruali Bluu nyeusi (darkblue) yenye rinda mbili na turn up isiyobana chini (upana kwa chini usipungue inch 7 na isizidi inch 8½ tai ndefu ya rangi ya suruali soksi ndefu nyeupe viatu vya ngozi nyeusi visigino vifupi na mkanda wa ngozi nyeusi.
- ii. Mashati meupe mikono mirefu 02 (tomato); iii. Viatu vya michezo (rubber au soccer boot). iv. Sare ya Michezo ni tracksuit nyeusi yenye mistari mieupe pembeni  
01
- v. Viatu vya shule ni nyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
- vi. Soksi jozi mbili nyeupe;
- vii. Mkanda nyeusi wa ngozi wa kuvalia suruali; viii. Sweta 01 (rangi bluu nyeusi) picha imeambatishwa;
- ix. Nguo za kushindia (shamba dress) suruali 02 (rangi nyeusi zenye rinda mbili na turn up chini);
- x. Tai 02 (bluu nyeusi);
- xi. Tisheti 02 (bluu nyeusi yenye nembo ya shule) zinapatikana shuleni 01@15,000/-;

2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

- i. Madaftari 07 (COUNTER BOOKS);
- ii. Ream (A4) ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
- iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatishwa);
- iv. Scientific Calculator;
- v. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe na vipimo kulingana na vipimo (upana ft 3 na urefu ft 6.
- vi. Mashuka Jozi 2 (rangi ya pinki), blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (rangi nyeupe);
- vii. Nguo za ndani za kutosha;
- viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe); ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
- x. Kwanja 1, jembe 1, mifagio 2 (hard bloom & soft bloom).
- xi. Pamoja na vifaa hivyo (x) kwa mwanafunzi wa HGK, HGL, HKL, HGFA na HGLI alete reki 1 na panga 1.
- xii. Sabuni ya maji lita 5 au aje na pesa TSh. 15,000 kwa ajili ya kununua sabuni hiyo.

ANGALIZO:

- BIMA ya afya ni muhimu sana kwa ajili ya matibabu ya mwanafunzi awapo shuleni hivyo Mwanafunzi aje na Bima ya afya ya Taifa (NHIF) kama ana bima na kama hana atatakiwa kuja na Kiasi cha Tsh. 50,400 kwa ajili ya kukatiwa bima hiyo.
- Mwanafunzi amepangiwa kuleta kifaa/vifaa kulingana na mazingira ya shule na tahasusi anayosoma.

### 2.3 Michango mbalimbali

#### a) Shule za Bweni

Na	Aina ya Mchango	Kiasi
1.	Mchango wa Uendeshaji wa Shule	65,000/=
3.	Tahadhari	5,000/=
4.	Nembo	5,000/=
5.	Kitambulisho cha Shule	5,000/=
	<b>Jumla</b>	<b>80,000/=</b>

Michango yote hapo juu ilipwe kwenye akaunti ya shule:

Jina la akaunti: TANDAHIMBA SECONDARY

Nambari ya akaunti: 71001200046 (NMB)

### 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

#### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

- Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
- Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
- Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

- ix. Kutunza mali za shule;
- x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
- xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUHIMU:

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;
- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;
- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

- 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:
- i. Wizi;
  - ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
  - iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
  - iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
  - v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
  - vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
  - vii. Kufuga ndevu;
  - viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
  - ix. Uvutaji wa sigara;
  - x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuo au kuolewa;
  - xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
  - xii. Kusababisha mimba;
  - xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
  - xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
  - xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
  - xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
  - xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
  - xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. Viambatisho na Fomu Muhimu

- i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
- ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
- iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
- iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....

MKUU WA SHULE




NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao).

Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule 0785 270 772
- Makamu Mkuu wa 0686 163 188



TAARIFA MUHIMU KWA MWANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO



SEHEMU A

Jina kamili la mwanafunzi (Herufi Kubwa) .....

Tarehe ya kuzaliwa.....

Jina la baba/mama/mlezi

..... Kazi yake

..... Namba ya simu.....

Anwani ya nyumbani..... Kijiji .....

KataTarafa.....Wialaya.....Mkoa.....

..... Dini/Dhehebu..... Email.....Uraia.....

SEHEMU B

Mambo unayopendelea kufanya mbali na masomo (Kwa mfano: Michezo, Bustani, Kushona, Kuchora n.k)

1..... 2.....

SEHEMU C : Ndugu wengine

No	Kiwango cha Elimu	Simu yake	Picha
1.			Passport size
2.			Passport size

SEHEMU D

Mimi .....Mzazi wa mwanafunzi  
..... Nimesoma na kuelewa sheria na kanuni za shule na kwamba nakubali  
kulipa ada na michango shule kama ilivyoainishwa. sahihi ..... Tarehe .....

SEHEMU E

Ninaahidi kuwa na tabia nzuri na mwenye bidii katika masomo yangu. Nimesoma maelezo yote na kuzielewa sheria za shule, na kwamba naahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Mungu nisaidie

Sahihi ya mwanafunzi ..... Tarehe

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**  
**PREME MINISTER' OFFICE -REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**



**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FORM**

**TO BE COMPLETED BY MEDICAL OFFICER (NAME)**

Student's full name ...

Age.....

I kindly request you to examine him physically and mentally if he is **fit or unfit** to pursue Advanced level studies in our school.

**PRELIMINARY INFORMATION BY THE STUDENT BEFORE THE DOCTOR.**

NO	DISEASE	YES/NO	NO	DISEASE	YES/NO
01	Tuberculosis (TB)		10	Epilepsy	
02	Pneumonia		11	Ear, Nose and throat	
03	Asthma		12	Skin disorder disease	
04	Heart trouble		13	Anemia	
05	Recurrent indigestion		14	Operations	
06	Jaundice		15	Serious accident	
07	dysentery		16	Eye disorder	
08	Kidney and urinary trouble		17	Venereal-disease	
09	Nervous breakdown				
<b>ADDITIONAL INFORMATION:</b>					

If any E.g; Physical defects (**Arm or leg impairments, chronic or family diseases**)

Etc .....

**I certify that he is fit/unfit to pursue education as stated**

Name

Signature

Station

Designation .....

Date:

**1. Jedwali Na. 1: Orodha ya Vitabu Vilivyoteuliwa kwa Ajili ya English Language Ngazi Sekondari ya Juu Kidato cha Tano na Sita**

Na.	Jina la Kitabu	ISBN	Namba ya Cheti	Mwaka	Kurasa	Mwandishi	Mchapishaji
1	Animal Farm	978-9966-25-898-4	1899	2024	117	George Orwell	East African Educational Publishers Ltd
2	Chasing the Leopard Finding the Lion	978-9987-08-178-3	1909	2024	329	Julie Wakeman-Linn	Mkuki na Nyota Publishers Ltd
3	The Opportunist	978-9987-763-01-6	1376	2023	227	Nyambari C. M. Nyangwine	Mbesa Books Distributors
4	The Horizon Unveiled	978-9987-483-19-8	1710	2011	237	Elite Fellowes Mwaisela	FGD Tanzania Ltd
1 (Play)	The Government Inspector	978-9966-46-440-8	1897	2024	166	Nikolai V. Gogol	East African Educational Publishers Ltd
2 (Play)	An Enemy of the People	978-9966-25-525-9	1907	2024	118	Henrik Ibsen	East African Educational Publishers Ltd
3 (Play)	A Taste of Heaven	978-9976-102-57-4	1388	2023	44	Farouk Topan	Mkuki na Nyota Publishers Ltd
1 (Poetry)	Summons: Poems From Tanzania	978-9976-1-0295-6	1401	2023	138	Richard S. Mabala et al.	Mkuki na Nyota Publishers
2 (Poetry)	Poets of Africa: Lament of the Silent & Other Poems	978-9966-25-337-8	1906	2024	167	Jared Angira	East African Educational Publishers Ltd

**2.**

**Jedwali Na. 2: Orodha ya Vitabu Vilivyoteuliwa kwa Ajili ya Literature in English Ngazi Sekondari ya Juu Kidato cha Tano na Sita**

Na.	Jina la Kitabu	ISBN	Namba ya Cheti	Mwaka	Kurasa	Mwandishi	Mchapishaji
1	Arrow of God	978-9966-46-792-8	1893	2024	248	Chinua Achebe	East African Educational Publishers Ltd
2	A Man of the People	978-9966-46-804-8	1892	2024	188	Chinua Achebe	East African Educational Publishers Ltd

3	A Grain of Wheat	978-9966-46-007-3	1365	2023	262	Ngugi wa Thiong'o	East African Educational Publishers Ltd
4	Petals of Blood	978-9966-46-094-3	1387	2023	357	Ngugi wa Thiong'o	East African Educational Publishers Ltd
5	No Longer at Ease	978-9966-46-000-4	1903	2024	164	Chinua Achebe	East African Educational Publishers Ltd
6	Joy Comes in the Morning	978-9987-08-153-0	1371	2023	187	Hopolang Phororo	Mkuki na Nyota Publishers Ltd
7	The Lion of Yola	978-9987-411-09-6	1547	2010	168	Severine Ndunguru	E&D Vision Publishing
1 (Play)	Betrayal in the City	978-9966-46-360-9	1390	2023	80	Francis Imbuga	East African Educational Publishers Ltd
2 (Play)	I Will Marry When I Want	978-9966-46-157-5	1389	2023	190	Ngugi wa Thiong'o & Ngugi wa Mirii	East African Educational Publishers Ltd
3 (Play)	Julius Caesar	978-9966-25-870-0	1896	2024	153	William Shakespeare	East African Educational Publishers Ltd
4 (Play)	Man of Kafira	978-9966-46-194-0	1902	2024	103	Francis Imbuga	East African Educational Publishers Ltd
1 (Poetry)	Boundless Voices: Poem From Kenya	978-9966-46-380-7	1894	2024	248	Arthur I. Luvai	East African Educational Publishers Ltd
2 (Poetry)	The Bleeding Heart and Other Poems	978-9987-483-10-5	1418	2009	135	Shilia Kaaya	FGD Tanzania Ltd

3.

***Jedwali Na. 3: Orodha ya Vitabu Vilivyoteuliwa kwa Ajili ya Kiswahili Ngazi ya Sekondari ya Juu Kidato cha Tano na Sita***

Na.	Jina la Kitabu	Namba ya Cheti	Mwaka	Kurasa	Mwandishi	Mchapishaji
1 (Riwaya)	Dunia Uwanja wa Fujo	1458	2023	250	Euphrase Kezilahabi	Africa Proper Education Network

2 (Riwaya)	Ua la Faraja	739	2007	406	W.E. Mkufya	Mangrove Publishers
3 (Riwaya)	Mirathi ya Hatari	1476	2023	96	C. G. Mung'ong'o	Mkuki na Nyota Publishers Ltd
4 (Riwaya)	Wasifu wa Siti Binti Saad	1479	2023	80	Shaaban Robert	Mkuki na Nyota Publishers Ltd
1 (Tamth)	Mukwawa wa Uhehe	1452	2023	187	M. M. Mulokozi	Africa Proper Education Network
2 (Tamth)	Shujaa Mirambo	1449	2023	119	Emmanuel Mbogo	Africa Proper Education Network
3 (Tamth)	Usaliti Mjini	1964	2024	103	Francis Imbuga	East African Educational Publishers Ltd
1 (Ushairi)	Fumbo Linaloelea	1486	2023	82	Nyambari C. M. Nyangwine	Mbesa Books Distributors
2 (Ushairi)	Malenga wa Ziwa Kuu	1960	2024	192	Wallah Bin Wallah	East African Educational Publishers Ltd
3 (Ushairi)	Andamo, Msafiri Safarini	1466	2023	114	Ghassani Mohammed Khelef	Educational Books Publishers Ltd
4 (Ushairi)	Wosia wa Baba	1943	2024	205	Amanzy Ahmed Mohamed	Abantu Publications Ltd

4.

***Jedwali Na. 4: Oroha ya Vitabu vilivyoteuliwa kwa Ajili ya Fasihi ya Kiswahili Ngazi ya Sekondari ya Juu Kidato cha Tano na Sita***

Na.	Jina la Kitabu	ISBN	Namba ya Cheti	Mwaka	Kurasa	Mwandishi	Mchapishaji
1 (Riwaya)	Vuta N'kuvute	9976-973-29-3	853	2007	248	Shafi Adam Shafi	Mkuki na Nyota Publishers Ltd
2 (Riwaya)	Asali Chungu	978-9966-46-901-4	1957	2024	148	Said Ahmed Mohamed	East African Educational Publishers Ltd
3 (Riwaya)	Mwana wa Yungi Hulewa	978-9966-46-868-4	1475	2023	145	Mohammed Said Abdulla	East African Educational Publishers Ltd

4 (Riwaya)	Vipuli vya Figo	978-9966-46-729-4	1959	2024	251	Emmanuel Mbogo	East African Educational Publishers Ltd
1 (Tamth)	Kaptula la Marx	978-9976-587-03-6	1487	2023	73	Euphrase Kezilahabi	Africa Proper Education Network
2 (Tamth)	Nyerere na Safari ya Kanaani	978-9987-701-56-8	1441	2023	91	Emmanuel Mbogo	Africa Proper Education Network
3 (Tamth)	Morani	9987-37-108-6	727	2007	55	Emmanuel Mbogo	Africa Proper Education Network
1 (Ushairi)	Dhifa	978-9976-587-07-4	1473	2023	80	Euphrase Kezilahabi	Africa Proper Education Network
2 (Ushairi)	Utenzi Majumui wa Karne ya 21	978-9987-37-006-1	1450	2023	89	Idd M. Nyambari Nyangwine	Mwimbe Publishers
3 (Ushairi)	Malenga wa Bara	978-9976-587-17-3	1438	2023	128	M.M Mulokozi na K.K Kahigi	African Proper Education Network
4 (Ushairi)	Fungate ya Uhuru	9987-37-159-0	723	2007	61	Mohamed Seif Khatibu	Africa Proper Education Network